Teacher.co.ke

**MUHULA WA PILI 2023**
**KISWAHILI**
**KIDATO CHA PILI (2)**
**MUDA: SAA 2 ½**

MWONGOZO

A. UFAHAMU

**a) i) Mwanaume**

Alikuwa na uwezo wa kuamua

Alistahili elimu ya juu

Ni mrithi

Ni kiongozi

Ni mwenye akili bora

Alithaminiwa kuliko mwanamke

Ni mshauri

**ii) Mwanamke**

Hatoi uamuzi

Hastahili kupata elimu ya juu

Hastahili kurithi mali, ufalme

Si kiongozi

Wa kuolewa

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Ni chombo cha kutamanika

Ni ngazi ya kujinufaisha

Ana akili dhaifu ana/akili duni

**b) i) Kwa nini mfalme aliwauliza wakwasi kwanza tafsiri ya kitendawili? (alamal)**

Waliaminika au walithaminiwa kuwa wenye ujuzi na maarifa.

Waliheshimiwa/nasaba bora/ukoo mzuri

Walikuwa washauri wakuu wa mfalme.

Alitarajia mmoja wao amuoe bintiye

*(Hoja yoyote iliyokamilika.)*

**ii) Kwa nini mfalme alishangazwa na jawabu la binti yake? (alama 2)**

Mfalme alitarajia dhamani ya tiba iwe kubwa

Kishaufu ni kitu duni

**c) "Akili ni nywele, kila mtu ana zake." Dhihirisha jinsi methali hii inavyobainika katika hadithi hii. (alama 4)**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

1. Mwanakishwira ana akili bora kuliko mfalme /wakwasi

2. Mchungaji alikuwanaakili nyingi kuliko mfalme.

3. Mwanakishwira na mchungaji walikuwa na akili nyingi kuliko wakwasi na mfalme.

*(Lazima pande zote mbili zilinganishwe wenye maarifa kila upande.)*

**d) Ni nini maoni yako kuhusu mwanaume aliyemwoa Mwanakishwira na kwa nini alikubali kuolewa na huyo. (alama 3)**

1. Mwanamume hana taasubi ya kiume.

2. Mchungaji ana akili sawana Mwanakishwira.

3. Mchungaji ndiye alitoa tiba ya ugonjwa wake.

4. Mmoja alifumba fumbo (Mwanakishwira) na mwingine akafombua (mchungaji).

*(Hoja yoyote moja.)* (alama 3)

e) i) Licha ya kuwa / bali na / zaidi ya kuwa / juu ya hayo / vile vile / pia / isitoshe / aidha /kuongeza.

ii) Akilalamika/akifuya/akihuzunika/akisononeka/ akiwa na uchungu uliopita kiasi

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

iii) Uzuriusiokifani/waajabu/mwingisana.

iv) Ukamshauri / akampa mawaidha / akamwosia / akamwangazia / akamwai nbia / akamwarifu.

## B. UFUPISHO

2. a) - Vijana wapendanao hulenga kuishi raha mustarehe.
- Kutiliana shaka kila wanapokuwa mbalimbali.
- Aghalabu hulaumiana
- Husameheana na kuendeleza mapenzi.
- Wakibahatika huoana.
- Hugundua ile raha ni ndoto tu.
- Uhalisia wa mambo ni kuvumiliana (5x1=5)

b) - Mwanasiasa hupigana awe mjumbe
- Achaguliwapo hatambuliwi kama bwana mkubwa.
- Huo ukubwa hutegemea mambo mengi / mengine / pesa, magari / sauti katika jamii.
- Msomi huanza bidii udogoni.
- Hulenga kutambuliwa kielimu.
- Husoma afikie kilele/daraja ya juu/shahada tatu kwa mfano.
- Akiajiriwa hugundua watu hawakijali kisomo chake / watu humwona mvivu.
- Mwanamziki hulaghaika kwamba akiongoza atapendwa na wengi.
- Anapofika kilele husahau kama ni binadamu wa kawaida.
- Huishia kujisikia mkiwa. (8x1=8)

Kumb: alama 2 ni za utirirko

## SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) /nd/, (2 x ½=1)

b) lau (1x1=1)

c) Walikuja -j-

Teacher.co.ke
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Alipewa -p- (2 x ½=1)

d) **<u>Ku</u>**ongea; kuunda kitenzi jina
a**<u>ji</u>**okoe; kuonyesha mtendaji wa kitendo (2x1=2)

e) Gari **hili hili** litanunuliwa. (1x2=2)

f) Hamjasoma wala kuelewa. (1x1=1)

g) Ng'ombe amesimama ndani ya zizi. (1x2=2)

h) Nomino; Mpaka wa Kenya na Somalia umefunguliwa.
kihusishi; Alifululiza mpaka nyumbani baada ya kazi. (2x1=2)

i) Alimdhulumu mwenzake vibaya.
Nilimsamehe makosa yake yote.
Wamehisi njaa tangu asubuhi.
kadiria( vingi huishia e, i, u) (1x1=1)

j) Kiima ni nomino inayotenda katika sentensi ilhali kiarifu ni sehemu inayotolewa maelezo katika sentensi. (1x1=1)

k) Wanyama hawa: ndovu, tembo na ngawa (wanyama wa pori) wote hupatikana mbugani. (1x1=1)

l) Kaa alifariki baada ya kuchomeka kwenye kaa. (1x2=2)

m) Wananchi hupenda nchi yao (taarifa)
Naomba kutumia kalamu yako (rai/ombi)
Wamemaliza kazi yote? (swali)
Ondokeni mara moja! (amri/agizo)
Lo! Amekula nyoka. (mshangao) (3x1=3)

n) Tu-;nafsi

-ta-;njeo/wakati

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

-lim-;mzizi

-a; kiishio/kauli tenda (4 x ½=2)

o.

i) enye ; Mtoto mwenye kalamu ataandika/ Mama mwenye kulea husifika.

ii) enyewe ; Mtoto mwenyewe ameandika. (2x1=2)

p. Mshale wake ulifungwa kwa unyoya mweusi (1x2=2)

q. Mama mzee; kirai nomino(RN)

chini ya mti; kirai kihusishi (RH) (2X1=2)

r. Kitabu kizuri sana kimesomwa leo

S-KN+KT

KN-N+V+E

N-kitabu

V-kizuri

E-sana

KT-T+E

T-kimesomwa

E-leo (8 x ½=4)

s. Mamake alikuwa mkali kwa sababu/ kwa kuwa/ kwani alikuwa mwanajeshi. (1x2=2)

t. Mzazi alisema kuwa hakutaka na asingetaka mtoto mkaidi kama yeye. (1x2=2)

u. Sikula kabla ya kumkama ng'ombe. (1x1=1)

v. PA; mahali karibu au panapodhihirika

KU; mahali mbali au kusikodhihirika

MU; ndani ya (3x1=3)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

**SEHEMU C: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**‘‘ Mhubiri Ashtumiwa Kwa Kuwapotosha Waumini’’**

Mhubiri mmoja mjini Changarawe ameshtumiwa vikali kwa kuwapotosha waumini katika kanisa lake kwa kuwapa mafunzo yenye utata...

a) Matangazo ya redio/ runinga/magazeti; matumizi ya hali isiyodhihirika ‘ashtumiwa’ (2x1=2)

**b)**

i. anwani/mada yenye mvuto; **‘‘ Mhubiri Ashtumiwa Kwa Kuwapotosha Waumini’’**
ii. Matumizi ya usemi wa taarifa; polisi walitaka kujua aliyowafunza waumini...
iii. vichwa/mada haizingatii sarufi kuokoa muda;Uchumi Yapanda-(gharama ya maisha)
iv. mada fupi na ya kuvutia
v. lugha sanifu
vi. matumizi ya vifupisho kv AFP
vii. hali isiyodhihirika
viii. Matumizi ya chuku
ix. lugha nyepesi kupasha ujumbe kwa watu wa matabaka yote
x. kuchanganya maelezo na tarakimu
xi. lugha inayotumika hutegemea taarifa inayotolewa (8x1=8)

*Mwanafunzi atoe mifano

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/